JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI UTAKAOFANYIKA TAREHE 13 SEPTEMBA, 2023 NA 14 SEPTEMBA, 2023

**Imetolewa na:**

**KATIBU MTENDAJI**
**12 SEPTEMBA, 2023**

**TAARIFA YA KATIBU MTENDAJI WA BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI UTAKAOFANYIKA TAREHE 13 SEPTEMBA 2023 NA 14 SEPTEMBA 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu Wanahabari,**

Tarehe **13 Septemba, 2023** na **14 Septemba, 2023** wanafunzi wa Darasa la Saba walioko Tanzania Bara katika jumla ya shule **18,320** watafanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (Primary School Leaving Examination - PSLE) 2023. Katika Mtihani huu, jumla ya watahiniwa waliosajiliwa ni **1,397,370** ambapo kati yao wavulana ni **654,652** sawa na asilimia **46.85** na wasichana ni **742,718** sawa na asilimia **53.15**.

Kati ya watahiniwa **1,397,370** waliosajiliwa kufanya mtihani mwaka 2023, watahiniwa **1,334,269** watafanya mtihani kwa lugha ya **Kiswahili** na watahiniwa **63,101** watafanya mtihani kwa lugha ya **Kiingereza** ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunzia. Aidha, watahiniwa wenye mahitaji maalum waliosajiliwa kufanya mtihani huo ni **4,583**, kati yao **101** ni wasioona, **1,321** wenye uoni hafifu, **1,125** wenye uziwi, **549** ni wenye ulemavu wa akili na **1,487** ni wenye ulemavu wa viungo.

## 2.0 MASOMO YATAKAYOTAHINIWA NA UMUHIMU WA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

**Ndugu Wanahabari,**

Katika mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, jumla ya masomo **sita (06)** yatatahiniwa ambayo ni **Kiswahili**, **English Language**, **Sayansi na Teknolojia/Science and Technology**, **Hisabati/Mathematics, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi/Social Studies and Vocational Skills** pamoja na **Uraia na Maadili/Civic**

**and Moral Education**. Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi ni muhimu kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla kwa kuwa hupima maarifa na umahiri wa wanafunzi katika masomo waliyosoma katika Elimu ya Msingi. Aidha, matokeo ya mtihani huu hutumika katika uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Sekondari. Hivyo, ni mtihani muhimu kwa wanafunzi, wazazi na jamii nzima kwa ujumla katika Taifa letu.

## 3.0 MAANDALIZI YALIYOFANYIKA

Maandalizi yote kwa ajili ya mtihani huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kusambazwa kwa karatasi za mitihani pamoja na nyaraka zote muhimu zinazohusu mtihani huo katika Halmashauri/Manispaa zote nchini. Aidha, maandalizi yote kwa ajili ya watahiniwa wenye mahitaji maalum yamefanyika ipasavyo.

Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri zimefanya maandalizi yote muhimu kwa kutoa semina kwa wasimamizi wa mtihani pamoja na kuhakikisha kuwa mazingira ya vituo vya mitihani yapo salama, tulivu na kuzuia mianya yote inayoweza kusababisha kutokea kwa udanganyifu.

## 4.0 WITO KWA KAMATI ZA MITIHANI, WASIMAMIZI, WAMILIKI WA SHULE NA JAMII

### 4.1 Wito kwa Kamati za Mitihani

Pamoja na maandalizi yote muhimu yaliyofanyika, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri zihakikishe kuwa usalama wa Vituo vyote vya mitihani unaimarishwa na kwamba Vituo hivyo vinatumika kwa kuzingatia Mwongozo uliotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

## 4.2 Wito kwa Wasimamizi

Baraza linatoa wito kwa wasimamizi wote walioteuliwa kusimamia mtihani kufanya kazi yao ya usimamizi kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu. Wasimamizi wahakikishe kuwa, wanafanya kazi ya usimamizi wa mtihani huu kwa weledi na kwa kuzingatia Kanuni za Mitihani na Miongozo waliyopewa ili kila mtahiniwa apate haki yake. Wasimamizi wahakikishe watahiniwa wote wanafanya mtihani kwa muda uliopangwa na katika hali ya utulivu.

Aidha, wasimamizi wahakikishe watahiniwa wenye mahitaji maalum wanafanya mitihani yao ipasavyo ili wapate haki yao ya msingi. Haki hizo ni pamoja na kuwapa mitihani yenye maandishi ya nukta nundu kwa watahiniwa wasioona na maandishi yaliyokuzwa kwa watahiniwa wenye uoni hafifu. Aidha, watahiniwa wenye mahitaji maalum waongezewe muda wa dakika **ishirini (20)** kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika **kumi (10)** kwa kila saa kwa masomo mengine, kama mwongozo wa Baraza unavyoelekeza.

## 4.3 Wito kwa Wanafunzi

Kwa **upande wa wanafunzi**, Baraza linaamini kuwa walimu wamewaandaa vizuri katika kipindi chote cha miaka saba ya elimu ya msingi. Hivyo, ni matarajio ya Baraza la Mitihani kuwa wanafunzi watafanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2023 kwa kuzingatia Kanuni za Mitihani. Aidha, Baraza halitarajii kuona mwanafunzi yeyote kujihusisha na vitendo vya udanganyifu. Mwanafunzi yeyote atakayebainika kufanya udanganyifu, matokeo yake **yatafutwa** kwa mujibu wa Kanuni za Mitihani.

### 4.4 Wito kwa Wamiliki wa Shule na Wakuu wa Shule

Baraza linawataka **Wamiliki wa Shule** kutambua kuwa shule zao ni vituo maalum vya mitihani na hivyo hawatakiwi kwa namna yoyote kuingilia majukumu ya wasimamizi wa mitihani katika kipindi chote cha ufanyikaji wa mtihani huu. Baraza halitosita kukifuta kituo chochote cha Mitihani endapo litajiridhisha pasipo shaka kuwa uwepo wake unahatarisha Usalama wa Mitihani ya Taifa. Aidha, **Wakuu wa Shule** watatekeleza majukumu yao ya usimamizi kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi uliotolewa na Baraza la Mitihani na kuepuka kuingilia usimamizi wa watahiniwa ndani ya vyumba vya mitihani.

### 4.5 Wito kwa Jamii

Baraza linatoa wito kwa **jamii kutoa ushirikiano unaotakiwa** katika kuhakikisha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2023 unafanyika kwa amani na utulivu. Wananchi wanaombwa kuheshimu eneo la mitihani na kuhakikisha kuwa **hakuna mtu yeyote asiyehusika** na mitihani anaingia kwenye maeneo ya shule katika kipindi chote cha mtihani. Kwa kufanya hivyo tutawawezesha watahiniwa waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa amani na utulivu.

## 5.0 HITIMISHO

Baraza la Mitihani la Tanzania linawaomba wananchi wote kutoa ushirikiano wakati wa uendeshaji wa mtihani ili watahiniwa wote wafanye mtihani katika hali ya utulivu. Aidha wananchi wote watoe ushirikiano katika kudhibiti vitendo vyovyote vya udanganyifu katika

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Baraza halitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kujihusisha au kusababisha udanganyifu wa mitihani kufanyika kwa mujibu wa Sheria za Nchi yetu.

Wadau wote wanaombwa kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini uwepo wa mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu wa mitihani wa aina yoyote ile. Taarifa za udanganyifu ziwasilishwe Baraza la Mitihani kupitia namba ya simu **0759360000** na barua pepe esnecta@necta.go.tz.

Baraza la Mitihani la Tanzania linawatakia watahiniwa wote kila la kheri katika kufanya mtihani huo tarehe **13 Septemba, 2023** na **14 Septemba, 2023**.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**



Dkt. Said Ally Mohamed

**KATIBU MTENDAJI**